

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU

07 JUNI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA AROBAINI NA TATU TAREHE 07 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

550. **MHESHIMIWA MOHAMMED SAID ISSA
(KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta unafuu wa gharama za michango ya kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza na cha Tano.

551. **MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA
(NANYAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa kukarabati majengo yaliyojengwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu Msingi.

552. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Halmashauri ngapi zimetekeleza agizo la Waziri Mkuu kununua dawa za viuadudu kutoka kiwanda cha Kibaha ili kutokomeza mazalia ya Mbu.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

553. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa dharura wa kudhibiti Mito inayopanuka na kuhatarisha maisha na mali za Wananchi katika Jimbo la Kawe.

WIZARA YA NISHATI:

554. MHESHIMIWA ZACHARIA PAULO ISSAAY (MBULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya upya tathimini ya maeneo kwenye Jimbo la Mbulu Mjini ambayo yalirukwa na Mradi wa REA I na II.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

555. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itawaunga Mkono *World Vision* kuendeleza ujenzi wa chuo cha VETA Choma.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

556. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Viwanda vya uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini.

WIZARA YA MAJI:

557. MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini ujenzi wa Mradi wa Maji wa Miji 28 utaanza kutekelezwa katika Wilaya ya Rorya.

558. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Wananchi wa Kijiji cha Mtila Kata ya Matola Njombe Mjini watapelekewa maji.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

559. MHESHIMIWA NORAH WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha Wadau wa Michezo kuwekeza katika kuzalisha Vipaji vya Michezo mbalimbali hasa mpira wa miguu.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

560. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itaongeza nguvu ya Mnara Kata ya Bukiko kutoka 2G hadi 3G na kuweka *Generator* kwani Kata hiyo ina shida ya mawasiliano.

WIZARA YA KILIMO:

561. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ipo tayari kuleta Wataalam Liwale kufanya utafiti kujua chanzo cha ugonjwa wa majani ya mikorosho kunyauka.

**562. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE
(KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itawapatia mbegu bora za Ufuta Wananchi wa Wilaya ya Kilwa waweze kuzalisha Ufuta mwingi kwani wanatumia mbegu za asili.

WIZARA YA MADINI:

**563. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE
(NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha uchimbaji wa Mbunyu unatekelezwa katika Kata ya Chiwata - Ndanda.

**DODOMA
07 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**